**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa shule : 0714928760**
**Makamu mkuu wa shule: 0687562646/0652177289**
**Shule ya sekondari Kisutu**
**S.L.P 20330**
**Kisutu, Dar Es Salaam.**

TAREHE…………………..

Mzazi /Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………………………………

S.L.P………………………………

…………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KISUTU HALMASHAURIYA JIJI LA DAR ES SALAAM, MWAKA 2024/2025**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katikashule hii mwaka ***2024/2025***, tahasusi ya ……………..

Shule ya Sekondari Kisutu ipo katikati ya jiji la Dar Es Salaam umbali wa kilometa 21 kutoka stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani-Magufuli (Magufuli bus Terminal).

Ukifika kituo cha mabasi cha Magufuli, panda magari yaendayo kwa haraka (**Mwendo kasi**) yaendayo Kivukoni nauli shilingi 1250, teremka kituo cha mwendokasi cha Kisutu, vuka upande wa kushoto wa barabara utaona soko la Kisutu, ifuate barabara hiyo mpaka kwenye makutano ya mtaa wa Kisutu na Mtendeni, elekea mtaa wa Kisutu utaona bango/kibao cha shule ya sekondari Kisutu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 03/07/2024 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni Tarehe 03/07/2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2024.

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**SHULE YA SEKONDARI KISUTU**

**TAARIFA ZA SHULE:**

Shule ya sekondari ya wasichana kisutu ipo mtaa wa kisutu, Posta, jijini Dar Es Salaam. Ili kufika shuleni ukitokea Mbagala, Gongo la Mboto, Chanika, Kinyerezi panda daladala iendayo Posta au kivukoni shuka kituo cha Akiba kilichopo barabara ya Bibi Titi. Vuka upande wa pili wa barabara hiyo ili kuingia mtaa wa Zanaki. Barabara ya kwanza kushoto kwako ni ya mtaa wa kisutu tembea mita chache na upande wa kushoto utaona bango kubwa la kibao cha shule. Iwapo utashuka Posta mpya vuka barabara hiyo na kukatisha kituo cha mafuta cha GBP (sheli ya GBP) songa mbele utaingia barabara ya upanga ukikatisha mbele utaingia mtaa wa kisutu tembea mpaka kwenye lango la shule. Shule ni ya kutwa pekee na masomo huanza saa 02:00 asubuhi hadi saa 08:20 mchana. Shughuli za masomo zinahusisha michezo na ziara za masomo. Walimu ni mahiri na wanaoipenda kazi yao.

**DIRA YA SHULE:**

Kuwa na elimu inayowezesha kufikiri kwa makini  na kutatua matatizo yaliyopo kwenye jamii muda wote.

**MALENGO YA SHULE:**

Kutoa elimu bora itakayotumika kujiendeleza na kuiendeleza jamii. Kwa kutumia teknolojia ya kisasa, mila bora zilizopo nchini katika ulimwengu huu wenye ushindani nakutoa mikakati itakayowezesha wanafunzi kuwa na afya ya mwili na akili ya kufanya maamuzi sahihi.

KAULI MBIU YA SHULE YETU NI **“ ELIMU KWA MAENDELEO**”

## A. MAHUDHURIO

1. Mwanafunzi lazima afike shuleni saa 1:00 asubuhi tayari kwa ukaguzi.
2. Mwanafunzi hatoruhusiwa kutoka katika eneo la shule ila kwa ruhusa ya Matron/mwalimu wa afya au mwalimu wa zamu. Inapokuwa lazima sana kutokana na waliotajwa hawapo, Mkuu wa Shule Msaidizi atatoa ruhusa.
3. Mzazi/Mlezi atapaswa kutoa maelezo endapo mwanafunzi hataonekana shuleni.
4. Ugonjwa lazima uthibitishwe na vyeti vya daktari.
5. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote katika ratiba yake.
6. Fedha za ada na michango zote zilipwe benki kwa wakati.
7. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kufuatilia maendeleo na mahudhurio ya mwanafunzi,pia kukagua notes na mazoezi ya masomo yote.

## B. MAMBO MUHIMU

Michango yote ilipwe katika Akaunti ya shule **NMB ILALA** nambari ya Akaunti **ni. 20301100078, Jina** la AKAUNTI ni **KISUTU SEC. SCHOOL** unaweza kulipia tawi lolote la NMB BANK.

Pamoja na taarifa hii pia napenda kukujulisha kuwa malipo yote yalipwe **bank** kama ilivyoainishwa kwenye jedwali bila kupungua. Original Bank pay slip iletwe kwa Mhasibu ikiwa na jina la mwanafunzi, kidato na mchepuo anaosoma.

**C. FEDHA**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 35,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**D. VIFAA KWA MATUMIZI BINAFSI:**

1. Begi la shule jeusi 1
2. Mkebe wa hisabati 1
3. Kamusi 1 ya kiingereza.
4. Madaftari kulingana na masomo (counter books quire 4)
5. Vitabu kulingana na masomo mwanafunzi anayosoma (orodha imeambatanishwa)
6. Koti jeupe lenye mikono mirefu kwa ajili ya mazoezi ya vitendo maabara kwa wale wanaosoma masomo ya sayansi (PCM, PCB, CBG)
7. Dissecting kit (kwa wanafunzi wa PCB na CBG-aina utaonyeshwa shuleni).

**E. SARE YA SHULE:**

**1.** Jezi 2 za viatu, raba nyeupe za kamba {**visizo na doa lolote**).
**2.** Jozi 2 za soksi nyeupe.
3. Mashati meupe mawili ya mikono mifupi/nusu kanzu kwa waislamu na juba.
4. Sketi mbili ndefu inazoishia kwenye kifundo cha mguu za rangi ya damu ya mzee (maroon).
5. Scarf yenye rangi ya sketi ya shule yenye mchirizi mweupe.
6. Nguo za michezo–**T-shirt yenye rangi ya bendera ya taifa na suruali ya track suit** yenye rangi ya bluu (**zitavaliwa wakati wa kipindi cha michezo tu**)
7. T-shirt ya shule (maelekezo utayapata shuleni).

**F. VIFAA VYA MATUMIZI YA SHULE:**

1. Kila mwanafunzi anapaswa kuleta karatasi za **rim mbili (2)** kwa mwaka.

**1.1 VIFAA VYA USAFI**

**PCB**-Ndoo na ufagio wa nje
**HGL**-Ufagio wa ndani, kikombe lita 1 na kizoleo
**CBG**-Brash ya chooni na dustibini kubwa
**HKL**-Moper na ndoo yake
**HGK**-Ndoo kubwa na squizer
**PCM**-Jembe na reki
**HGLi**-Spring file dazeni moja na dumu la lita tano la sabuni ya maji aina ya ‘Lit’.

**G. MALI ZA SHULE:**

Mwanafunzi hukabidhiwa vitabu vya kusoma, dawati pamoja na kiti. Pia anaweza kukabidhiwa mali za shule katika nyakati mbalimbali, ni wajibu wake kutunza vifaa hivi na lazima virudishwe pale atakapotakiwa kufanya hivyo. Mwanafunzi atakayeshindwa kurudisha kifaa chochote itabidi alipe gharama zake. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kudumisha nidhamu ya hali ya juu.

**H. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:**

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na usagaji.
3. Ulevi
4. Uvutaji bangi, na matumizi mengine ya madawa ya kulevya.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya taifa.
8. Kuolewa.
9. Kupata mimba au kutoa mimba
10. Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kuwa na simu shuleni
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.

**I. MWANAFUNZI ATAONYWA KATIKA NGAZI ZIFUATAZO:**

1. Mwalimu wa darasa.
2. Mwalimu wa nidhamu.
3. Mwalimu wa malezi
4. Mkuu wa shule.
5. Kikao cha Bodi ya shule.

**J. TAARIFA ZA MAENDELEO:**

Taarifa za maendeleo ya wanafunzi hutolewa mara mbili kwa mwaka. Mzazi/Mlezi hakikisha unatoa taarifa na anuani sahihi. Ikiwa kuna badiliko lolote la anuani, ni wajibu wa mzazi au mlezi kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi/binti yake. Palipo na tatizo wasiliana au toa taarifa mapema kwa mkuu wa shule.

**FOMU IJAZWE NA KUREJESHWA SHULENI**
**NI MUHIMU KUKAMILISHA FOMU HII**
**FOMU YA MAPOKEZI**

| |
|---|
| ***Picha ya mwanafunzi*** |

A. IJAZWE NA MWANAFUNZI
1. Jina la mwanafunzi……………………………………………………………………………
2. Taifa……………………………………………………………………………………………
3. Raia……………………………………………………………………………………………
4. Dini……………………………………………………………………………………………
5. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………
6. Shule ya msingi/Sekondari uliyotoka…………………………………………………
7. Tarehe ya kutoka shule hiyo…………………………………………………………………

……………………………
SAHIHI YA MWANAFUNZI

| |
|---|
| ***Picha ya mzazi*** |

**B. IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**
1. Jina kamili la baba/mlezi…………………………………………………………………
Anuani kamili mjini Dar-es-salaam……………………………………………………………………………..
Namba ya simu………………………………….. /…………………………………….
Sehemu anapoishi:
mtaa…………………………………kata……………………….wilaya……………………..
Namba ya nyumba…………………………….Namba ya simu ya ofisini…………………………
No. ya simu ya nyumbani…………………………… No. ya simu ya ndugu……………………………….

2. Jina kamili la mama mzazi/mlezi………………………………………………………………………………
Anuani kamili mjini D'salaam…………………………………………………………………………………….
Namba ya simu………………………………….. /…………………………………….
Sehemu anapoishi:
mtaa…………………………………kata……………………….wilaya……………………..
Namba ya nyumba…………………………….Namba ya simu ya ofisini…………………………
No. ya simu ya nyumbani…………………………… No. ya simu ya ndugu…………………………

MAELEZO YA KIKAZI
Jina la mwajiri wa idara………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………………….
Anuani…………………………………………………No. ya simu……………………………………………..
Mahali ofisi ilipo……………………………………kazi ya mzazi/mlezi……………………………

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI…………………………………………..

# SHULE YA SEKONDARI KISUTU
# S.L.P 20330
# DAR-ES-SALAAM
# SIMU: 0714928760

**CHETI CHA KUPIMA CHA MWANAFUNZI KIJAZWE NA MGANGA MKUU WA HOSPITALI YOYOTE YA SERIKALI**

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………………
KIDATO…………………………………………… UMRI…………………………………………

Hii ni kuthibitisha kwamba nimempima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Maoni yangu **ANAFAA/HAFAI** kuendelea na masomo yake /anahitaji matibabu kabla ya kumruhusu kuendelea na masomo yake

**Maelezo ya afya:**
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………..

| ………………………… | ………………………… | …………………… |
|---|---|---|
| Sahihi ya daktari | Muhuri | Tarehe |

Kama mwanafunzi ana matatizo ya afya, tafadhali, Daktari elezea matokeo ya kupimwa kwa siri/au wazi kwa anuani iliyo hapo chini.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KISUTU
S.L.P 20330
DAR-ES-SALAAM

GENERAL STUDIES

1. GENERAL STUDIES FOR FORM FIVE AND SIX (THE BEST GUIDE TO PASS A-LEVEL EXAMINATIONS)
   BY Maisha Mwaipaja
2. GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL CERTFICATE (FORM FIVE) BY Mbalase, R, F.R
3. UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL, BY Birigwamungu, J AND Deogratias, M.S 4TH EDITION DAR-ES-SALAAM

BIOLOGY

1. BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK FORM FIVE (Tanzania Institute of Education)
2. BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK FORM SIX (Tanzania Institute of Education)
3. BIOLOGICAL SCIENCE 1& 2 (D. J TAYLOR, N.P.O GREEN G. W STOUT)

HISTORY

1. ESSENTIAL IN ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 1 BY SALEHE YASSIN
2. ESSENTIAL IN ADVANCED LEVEL HISTORY PAPER 2 BY SALEHE YASSIN

KISWAHILI

1. KISWAHILI KIDATO CHA TANO NA SITA-OXFORD UNIVERSITY PRESS
2. FASIHI
   1. RIWAYA – i) VUTA NIKUVUTE ii) MFADHILI
   2. TAMTHILIA- i) NGUZO MAMA ii) MORANI
   3. USHAIRI- i) FUNGATE YA UHURU ii) CHUNGU TAMU

ENGLISH LANGUAGE

1. ADVANCED ENGLISH LANGUAGE 5&6 OXFORD UNIVERSITY
2. SELECTED POEMS
3. AN ENEMY OF THE PEOPLE –HENRIK IBSEN
4. BETRAY IN THE CITY- FRANCIS IMBUGA
5. I WILL MARRY WHEN I WANT-NGUGI WA THIONG'O
6. THE BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN – AYI KWER ANNAH
7. HIS EXCELLENCY THE HEAD OF STATE – DANNY SAFO
8. A MAN OF THE PEOPLE – CHUNUA ACHEBE

BASIC MATHEMATICS DEPARTIMENT

1. BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS; FORM FIVE AND SIX, BY TIE.
2. BASIC APPLIED MATHEMATICS. ADVANCED SECONDARY SCHOOLS, FORM FIVE, BY SEPTINE I. SILLEM

3. ADVANCED MATHEMATICS FOR SECONDARY SCHOOLS. FORM FIVE, BY SETINE SILLEM ESSENTIALS FOR A-LEVEL PURE MATHEMATICS; FORM 5 CURRENT SYLLABUS; BY TELEMU MAJIGWA.

GEOGRAPHY BOOKS LIST:

1. PHYSICAL GEOGRAPHY; BY MSABILA
2. PHYSICAL GEOGRAPHY; BY ZISTI KAMILI
3. PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAMS BY R B BANNET
4. HUMAN AND ECONOMICS GEOGRAPHY. BY ZISTI KAMILI
5. AN INTEGRATED REGIONAL STUDY ON HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY. ADVANCED PAPER 2 BY D.T MSABILA
6. GEOGRAPHY AN INTERGRATED APPROACH BY DAVID WAUGH
7. PRINCIPLE OF PHYSICAL GEOGRAPHY BY FR. MONKHOUSE
8. PRACTICAL GEOGRAPHY ALIVE, MAP READING, PHOTOGRAPHY, FIELD, STATISTICS AND INTRODUCTION TO SURVEY BY ZISTI KAMILI.
9. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA BY JOHN M. PRICHAD

CHEMISTRY BOOKS LIST.

1. S.K JAIN (2006) CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI. HINDU COLLEGE UNIVERSITY OF DELHI
2. S.K JAIN (2006) CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XII. HINDU COLLEGE UNIVERSITY OF DELHI
3. ESSENTIALS OF PHYSICAL CHEMISTRY BY BAHL AND TULI, S. CHAND
4. GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL, STUDENT BOOK FOR FORM FIVE AND SIX (TIE).
5. PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL, STUDENT BOOK FOR FORM FIVE AND SIX (TIE).
6. INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL, STUDENT BOOK FOR FORM FIVE AND SIX (TIE).
7. ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL, STUDENT BOOK FOR FORM FIVE AND SIX (TIE).
8. ADVANCED PHYSICAL CHEMISTRY BY NGAIZA.
9. ORGANIC CHEMISTRY MZUMBE PROJECT, PART A AND B
10. PHYSICAL CHEMISTRY MZUMBE PROJECT.

PHYSICS BOOKS LIST

1. PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL STUDENT BOOK, FORM FIVE (TIE)
2. PRINCIPLES OF PHYSICS, S. CHAND CLASS XI
3. ADVANCED PHYSICS, NELKON AND PARKER
4. PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL STUDENT BOOK, FORM SIX (TIE)
5. PRINCIPLE OF PHYSICS, S. CHAND CLASS XII.

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumezuka tabia ya utapeli/wizi kwa njia ya mtandao. Baadhi ya wazazi/walezi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kuwa ni walimu na kuafahamisha wazazi/walezi kuwa motto wa mzazi/mlezi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi/mlezi atume pesa.

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZA SIMU ZILIZOPO KWENYE FOMU HII.**